


TAASISI YA TEKNOLOJIA DAR ES SALAAM

TAARIFA KUHUSIANA NA MITIHANI YA KWANZA YA MAJARIBIO (Continuous Assessment Tests I) YA TAASISI ILIYOPANGWA KUFANYIKA TAREHE 19-23 DESEMBA, 2016

- 1) Leo (16/12/2016) Waziri wa Elimu wa Serikali ya Wanafunzi ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DITSO) alitoa tamko lenye kichwa cha habari “KUTOITAMBUA KISHERIA RATIBA YA MITIHANI YA MAJARIBIO”. Katika tamko hilo alitoa madai yafuatayo:
 - a) Kipengele cha prospectus 5.10.1 kinachosema “*Dates and times of conducting continuous assessments shall be determined and indicated by the respective Lecturer(s)/Instructor(s) in the course outlines or study guides or otherwise at the beginning of the Semester.*” kimekiukwa
 - b) Ratiba ya mitihani iliyotolewa ina mapungufu
- 2) Inasisitizwa kuwa hakuna ukiukwaji wowote wa kipengele cha prospectus 5.10.1 kama inavyodaiwa. Ratiba ya mitihani ya kwanza ya majaribio imepangwa kufanyika tarehe 19-23 Desemba, 2016 kulingana na *Almanac* ya Taasisi ya mwaka 2016/17; iliyopata idhini ya kikao cha 75 cha Bodi ya Taasisi kilichokaa tarehe 22 Septemba, 2016 na kuwekwa kwenye tovuti ya Taasisi tarehe 1 Oktoba, 2016.
- 3) Kwa kuzingatia ufafanuzi uliotolewa hapo juu, kila mwanafunzi wa Taasisi anaagizwa kuzingatia yafuatayo:
 - a) Mitihani ya kwanza ya majaribio ya semesta ya kwanza, 2016/17 itafanyika tarehe 19-23 Desemba, 2016 kama

inavyoelekezwa kwenye *Almanac* ya Taasisi na kulingana na ratiba ya mitihani ambayo imetolewa. Kuacha kufanya mitihani hii bila kuruhusiwa rasmi kulingana na Kanuni za Taasisi kutahesabika kuwa ni “*Abscondment*”

- b) Pale ambapo kuna ulazima wa kufanya mabadiliko ya ratiba ya mitihani iliyotolewa, mabadiliko hayo yafanyike chini ya uratibu wa Mkuu wa Idara husika. Hata hivyo, ni lazima mitihani yote ya majaribio ya kwanza ya semesta hii iwe imekamilika ifikapo tarehe 30 Desemba, 2016.
- c) Kwa vile inafahamika kuwa kuna baadhi ya wanafunzi ambao wamekamilisha usajili na hawajapata vitambulisho, wanafunzi wote wanaruhusiwa kufanya mitihani ya majaribio ya kwanza ya semesta hii, lakini matokeo yatatolewa tu kwa wale watakaokuwa wamekamilisha usajili wao.
- d) Kama zilivyo kanuni za mitihani, kila mwanafunzi anatakiwa kuwasili kwenye chumba cha mtihani (iwe ndani ya Taasisi au katika kituo cha Shule ya Msingi Kisutu) nusu saa kabla ya muda uliopangwa wa mtihani husika kuanza.
- e) Kanuni zingine zote zinazotawala Mitihani ya Taasisi zitazingatiwa.



ROY R ELINEEMA
MSAJILI

Cc: Mkuu wa Taasisi, DPARC, DPAF, LO, Wakuu wa Idara, Msarifu, Mshauri wa Wanafunzi, EO, AO, DITSO, Mbao za matangazo